

| Bean SMS for March-April bean campaign (Developed in Arusha SG Hotel 21-23rd Feb) | | | | |
|---|--------------|---------------|---|-----|
| | When to Send | Where to send | | |
| Introduction Messages | 14/03/17 | All districts | Kuungeze mavuno kwa ajili ya chakula, lishe na soko, Wizara ya Kilimo kupitia kituo cha utafiti Selian, wadau kama CABI, FRI, Esoko na wahusika wengine wa kilimo cha maharage Tanzania wameadaa jumbe fupi na vipindi vya radio vyenye taarifa za uzalishaji maharage kwa kutumia kanuni bora za kilimo kama matumisi ya mbegu zilizoboreshw. Kupokea jumbe ni bure. Sikiliza SAUTI YA INJILI-Ijumaa na Jumapili saa1:15 usiku, SAFINA FM Ijumaa 12:30-1:00 na Jumapili saa2:30-3:00 usiku | 478 |
| Matumizi ya mashine | 14/03/18 | All districts | Msimu umeanza, tayarisha shamba kutumia trekta, pawa tila au jembe la kukokotwa na wanyamakazi-kurahisha kazi, kuoko muda na kuruhusu maji kupenya kwa urahisi | 159 |
| Matumizi ya viuagugu | 15/03/18 | All districts | Iwapo shamba limeota magugu kabla hujapanda tumia kiuagugu kama touchdown, roundup, Guguset n.k kupunguza gharama ya kurudia kulima. Pata ushauri wa Afisa Ugani | 160 |
| Seed selection | 15/03/18 | All districts | Panda maharage kulingana na mazingira, msimu na mfumo(mseto/siyo mseto)wa kilimo wa eneo lako. Kila mfumo unahasara na faida zake. Kwa ushauri muone Afisa Ugani | 160 |
| Kilimo mseto | 15/03/18 | All districts | Faida za kilimo mseto:- kurutubisha udongo,kutunza unyevu na kupunguza magugu, mbegu zenye tija ni Jesca(Punda), Lyamungo 85, 90, Selian 94 na Njano gololi | 156 |
| Kilimo mseto | 15/03/18 | All districts | Katika kilimo mseto,kuna teknologia kama kupanda maharage baada ya mahindi kuota- kurahisisha palizi na uotaji wa mahindi. Pili nikupanda zote kwa wakati mmoja | 160 |
| Nafasi za upandaji katika kilimo kisicho cha mseto | 16/03/18 | All districts | Ukanda wa kati na juu, panda Maharage aina ya Seliani14/15(ya kamba/muda mrefu na yana madini ya chuma na zinki), Njano Uyole(Njano dume). Kukomaa siku 85-110 | 129 |
| Nafasi za upandaji katika kilimo mseto | 16/03/17 | All districts | Kilimo kisicho cha mseto unashauriwa kupanda maharage kwa kipimo cha sm50 kati ya mistari na sm20 shimo hadi shimo, weka mbegu 2 | 160 |
| Seed selection | 16/03/18 | All districts | Kulima mseto panda mahindi umbali wa sm75 mstari kwa mstari na 50 shimo kwa shimo mbegu 2, Panda maharage kati ya mstari wa mahindi sm20 shimo kwa shimo 158 mbegu 2 | 158 |
| Seed selection | 17/03/18 | All districts | Kwa maeneo ya mvua chache, tumia mbegu bora za maharage zinazokoma mapema, kati ya siku 67-80 mfano-JESCA(kijivu/kombati/Punda), Selian 12 na Selian13 (gololi) | 160 |
| Seed selection | 17/03/18 | All districts | Ukanda wa kati-Lyamungu85, 90(Rosecoco, Nyayo), Jesca na Njano Uyole. Aina hizi huhistamili magonjwa yanayosabishwa na fangasi(Chule,Baka pembe, kutu ya majani) | 160 |
| Seed selection | 17/03/18 | All districts | Pia unaweza tumia mbegu za maharage zinazotambaa (za kamba) na zinazozaa zaidi-Selian 05, Selian 06 na Cheupe kwa ukanda wa juu. Kukomaa ni kati ya siku 90-110 | 159 |
| Sababu na wakati | 20/03/18 | All districts | Kama udongo hauna fosforas ya kutosha, weka mfuko 1 sawa na 50kg/ekari-DAP au mifuko 2 na nusu sawa na 150kg/ekari-NPK au Minjingu phospahte kupata mavuno mengi | 160 |
| Namna ya kutumia mbolea husika, (viwandani na samadi) | 20/03/18 | All districts | Chimba shimo sm10, weka mbolea kifunko kimoja cha soda na urudishie udongo ili mbegu isigusane na mbolea, weka maharage na ufukie. Pata ushauri wa Afisa Ugani | 159 |
| Nyenko za ushauri wa viwango vya mbolea | 20/03/18 | All districts | Kwa ushauri wa aina na matumizi sahihi ya mbolea, wasiliana na Afisa Ugani. Wengi wamefudishwa na wana ujuzi wa nyenko ya ushauri wa viwango vya mbolea (FOT/NE) | 160 |
| Dynamic | 21/03/18 | All districts | Kwa uwezo mdogo wa simu yako kuhifadhi jumbe zote za kilimo unazopokea, tunza kwa kuzinakili kwenye daftari lako la kumbukumbu ili kujikumbusha inapohitajika | |
| Farm records | 22/03/18 | All districts | Hakikisha unatunza kumbukumbu za uzalishaji (Pembejeo, nguvu kazi, tarehe za shughuli),be, mapato na matumizi ili kujua faida na hasara za kilimo cha maharage | |
| Farm records | 23/03/18 | All districts | Hakikisha nguvu kazi ya familia inaingizwa kwenye kumbukumbu za gharama za uzalishaji ili kupata uhalisia wa mapato na matumizi ya kilimo chako. Andika na uwewe | |
| Sababu za kuweka matandazo shambani (Mulching) | 26/03/18 | All districts | Kwenye kilimo cha maharage, ni muhimu kutandaza masalia ya mazao jamii ya mikunde kuhifadhi unyevu na kuboresha rutuba ya udongo wa shamba lako | |
| FROM APRIL | | | | |
| Scouting | 9th april | All districts | Kagua shamba lako mara kwa mara ili kubaini uwepo wa visumbu vya mimea na kuchukua hatua sitahiki, kwa maeleo zaidi wasiliana na mtaalam wa kilimo | 149 |
| Weeding | 10th April | All districts | Kwa mavuno zaidi, fanya palizi wiki 2-3 baada ya maharage kuota ili kupunguza ushindani kati ya maharage na magugu kwa virutubisho muhimu vya mimea na unyevu | 157 |
| Weeding | 11th April | All districts | Kudhibiti magugu kwenye shamba la maharage kwa kutumia viuagugu huokoa muda na gharama kulinganisha na palizi la mkono. Kwa maeleo Pata ushauri wa Afisa Ugani | 160 |
| Weeding | 12th April | All districts | Kwenye shamba lilipopandwa maharage peke yake, viuagugu kama Amazone 250 EC, Sateca 150 SL, Bean clean15.5% EC na Basagran 480EC vinatumika kudhibiti magugu | 156 |
| Safe use of chemicals | 12th April | All districts | Linda afya yako-fuata kanunu bora za utumiaji wa viuatilifi. Safisa pumpu vizuri kabla na baada ya kutumia, kuepuka madhara yatokanayo na kuchanganya viuatilifi | 160 |
| Fall armyworm control | 16th April | all districts | Kuna mdudu hatari anayeharibu mahindi aitwaye Kiwavi vamizi. kichwani ni kama herufi Y nyeupe iliyogeuzwa chini. Ana madoa 4 meusi yaliyopangwa kimraba mkiani | 158 |
| Fall armyworm control | 17th April | all districts | Kagua mimea yako hasa mahindi mara mbili kwa wiki. Dalili za viwavi ni mashimo madogo, makubwa na vitu kama vumbi ya mbao ya rangi ya chungwa kwa matawi. | 155 |
| Fall armyworm control | 18th April | all districts | Pulizia viuatilifi vya kuua viwavi vamisi mapema akiwa kwenye hatua zake za awali kabla viwavi hawaja ingia na kujificha ndani ya mmea wa mahindi . | 149 |
| Fall armyworm control | 18th April | all districts | Tumia viuadudu kama Duduba 450 EC,mupacrone 500 EC,match save au PROTRINE 60 EC. Weka cc 3 kwa lita moja ya maji, changanya vizuri. Muone mtaalamu wa kilimo | 156 |

| | | | | |
|----------------------------------|---------------|---------------|---|-----|
| Pest and diseases | 8th May 2018 | all districts | Dhibiti magonjwa ya fangasi (chule) kwenye shamba la maharage-Dalili ni madoa meusi katika mishipa ya majani na kunyauka kwa mifuko ya maharage | 143 |
| Pest and diseases | 8th May 2018 | all districts | Dhibiti magoija ya bakajani, bakapembe, kutu na chule kwa kutumia viuakuvu kama Benomil, Blue copper, Ivory, chlorothalonil au ridomi.Waasiliana na afisa kilimo | 160 |
| Pest and diseases | 9th May 2018 | all districts | Bakajani tangulia na bakajani chelewa ni husababishwa na kuvu. Dalili-madoa kwa majani, shina na shina la maua,kuanguka kwa majani na hasara kubwa ya mavuno | 156 |
| Pest and diseases | 9th May 2018 | all districts | Kudhibiti Bakajani tangulia na chelewa- lima kwa mzunguko angalao mwaka mmoja, ondoa mimea ya kujiotea na kwekwe, ng'oa mimea iliyo ambukizwa na uondoe masalia | 160 |
| Pest and diseases | 10th May 2018 | all districts | Halo blight ni ugonjwa wa bakteria. Dalili zake ni kama za blight ya maharage. Zua na udhibiti kama iliyo elezwa kwenye blight. Waasiliana na afisa kilimo | 156 |
| Pest and diseases | 10th May 2018 | all districts | Ugonjwa wa maharagwe wa blight husababishwa na bakteria.Dalili-madoa kwa majani, mashina na mifuko ya mbegu. Mbegu huambukizwa ndani na njie | 140 |
| Pest and diseases | 11th May 2018 | all districts | Ugonjwa wa maharage wa blight huenea sana kupitia mvua yenye upepo wa kuvuma, maji yanayotiririka ardhini, watu, mashine na wadudu wanaopitia kwenye mimea | 154 |
| Pest and diseases | 11th May 2018 | all districts | Kuzuia blight kwenye maharage-Fanya kilimo mzunguko kubadilisha na mahindi kila miaka 2-3, usiingie shambani wakati majani yana unyevu. Weka shamba likiwa safi | 159 |
| Pest and diseases | 12th May 2018 | all districts | Dalili ya ugonjwa wa virusi kwenye maharage ni majani kujikunja na mmea kudumaa, ng'oa na uchome/kufukia mmea ulioathirika. kwa maelezo wasilana bwana shamba | 157 |
| Pest and diseases | 12th May 2018 | all districts | Weka shamba lako la maharage katika hali ya usafi ili kuzuia kasi ya kuenea kwa magonjwa na wadudu waharibifu | 109 |
| Pest and diseases | 14th May 2018 | all districts | Dhibiti wadudu waharibifu wa maharage (funza, mbawakavu, sota) kwa kutumia viuatilifu kama Karate, Duduall, Thunder, Dusban, Thionex, Dudubar au Selecron nk | 157 |
| Pest and diseases | 14th May 2018 | all districts | Funza wa vitumba ni nondo mharibifu wa maharage. Viwavi hula vitumba na maua.Huingi ndani ya mifuko ya maharage na kuacha tundu kwenye mfuko na kuharibifu mbegu | 134 |
| Pest and diseases | 14th May 2018 | all districts | Kudhibiti Funza wa vitumba-panda mapema, tumia kilimo mseto na cha mzunguko. Tumia viuadudu mfano Dudu All, Ambush, Bulldock. Soma maelekezo kwenye kifungashio | 159 |
| Pest and diseases | 15th May 2018 | all districts | Kimamba na vithiripi wa maua:hawa ni wadudu waharibifu wa maharage inapokua shambani, atharri za wadudu ha huwa kubwa zaidi kipindi cha mvua nyangi | 159 |
| Pest and diseases | 15th May 2018 | | Tumia Viuadudu kama Rogor au sumithion kudhibiti kimamba na vithiripi. Weka cc 20 (vijiko 4 yya chai) kwa lita 15 za maji ndani ya bomba. Soma kifungashio | 160 |
| Pest and diseases | 16th May 2018 | | Dhibiti viwavi jeshi vamisi mapema akiwa kwenye hatua zake za awali kabla viwavi hawaja ingia na kujificha ndani ya mmea wa mahindi . | 143 |
| Pest and diseases | 16th May 2018 | all districts | Tumia viuadudu kama Duduba 450EC,mupacrone 500EC,match save au PROTRINE 60 EC. Weka cc 3 kwa lita moja ya maji, au cc 60 kwa pampu ya lita 20. changanya vizuri | |
| Pest and diseases | 17th May 2018 | all districts | Linda afya yako-fuata kanunu bora za utumiaji wa viuatilifu. Safisa pumpu vizuri kabla na baada ya kutumia, kuepuka madhara yatokanayo na kuchanganya viuatilifu | 157 |
| Pest and diseases | 17th May 2018 | all districts | Mahindi-pulizia viuadudu kwenye mmea wote, matawi ya njie na kwenye mhindi juu (funnel) ambapo viwavi wanajificha.Kaguu na kufuatilia baada ya siku 7. | 109 |
| Pest and diseases | 18th May 2018 | all districts | Pulizia asubuhi au jioni, wakati viwavi wanashambulia mimea. Usipulizie wakati juu ni kali, upepo ni mwingu au dalili za mvua. Wasiliana na mtaalamu wa kilimo | 157 |
| Pest and diseases | 18th May 2018 | all districts | Viuadudu hivi vinafanya kazi kwa njia sawa,usichanganye-tumia kimojawapo kinachopatikana karibu nawe. Pulizia kwa wakati na kwa vipimo sahihi. | 159 |
| Pest and diseases | 21st May 2018 | all districts | Ukizingatia kanunu bora za kilimo kwenye maeneo ya mvua nyangi, maharage kamba huzaa vizuri kutoka chini hadi juu na kutoaa mavuna katy ya magunia 6-30 kwa ekari | 160 |
| Pre-harvest-third weeding | 12/06/18 | all districts | Weka shamba lako katika hali ya usafi kwa kung'olea magugu.Hii inasaidia kuondoa maficho ya wanyama waharibifu, maharage kukauka vizuri na kurahisisha uvunaji | 159 |
| Pre-harvest | 13/06/18 | all districts | Kabla ya kuvuna, andaa vifaa nya kuvunua na kuhifadhi maharage kama mifuko, mapipa, maturubai ya kuanikia. Safisha chumba cha kuhifadhi na kupuliza viuadudu. | 159 |
| Pre-harvest | 14/06/18 | all districts | TAHADHARI-Viuadudu nya maji maji kama Actellic50EC/ShumbaSuper 50EC vizitumike kupulizia nafaka wakati wa kuhifadhi.Vina sumu kali na hutumika kuosha ghal tu | 158 |
| Dynamic-record keeping | 15/06/18 | all districts | Kumbuka kutunza kumbukumbu za uzalishaji-Pembejeo, nguvu kazi ya familia, bei/tarehe za shughuli, mapato na matumizi, n.k, kujua faida na hasara za kilimo chako | 160 |
| Harvest | 16/06/18 | all districts | Tumia kanunu bora za kuvuna maharage ili kupunguza upotevu na kutunza ubora wake. Ng'oa maharage wakati wa asubuhi kabla jua halijakua kali.Usivune kwa mvua | 156 |
| Harvest-drying | 18/06/18 | all districts | Usianike maharage ardhini kwa kuwa yanapoteza ubora, yatandaze kwenye turubali, mkeka au juu ya kichanja ili yakaake juani tayari kwa kupura (kupigapiga) | 154 |
| Harvest-drying | 19/06/18 | all districts | Kupata mavuno bora ya maharage, yakaushe vizuri na kuyapigapiga kwa kutumia fito ya wastani hii itacongeza thamani ya zao kwa kuepusha punje kupasuka/kuvunjika | 159 |
| Harvest-drying | 20/06/18 | all districts | Kukaushia maharage ardhini husababisha kuoza na kuliwa na mchwa hivyo kupunguza mavuno na kushusha ubora. Kausha maharage bilä kugusana na ardhi | 144 |
| Scouting | 21/06/18 | all districts | Endelea kugagua mahindi yako kwenye shamba la maharage. Usitumie viuadudu nya kudhibiti viwavi vamizi baada ya mahindi kutoa mbelewele/yanachanua | 152 |
| Storage | 12/07/18 | all districts | Hifadhi maharage makavu kwenye ghala, pipa, madumu au mifuko ya PICS kuepuka gharama za kutumia viuatilifu, kushambuliwa na wadudu na kulinda usalama wa mbegu | 159 |
| Storage | 13/07/18 | all districts | Ni muhimu kutumia dawa za kuhifadhi chakula/mbegu kama mazao yanahifadhiwa kwenye mifuko ya kawaida kuzuia wadudu waharibifu kushambulia maharage kwenye ghala | 158 |
| Marketing | 14/07/18 | all districts | Jiunge na vikundi nya uzalishaji.Maharage yaliyo fungashwa, yana taarifa kama aina, uzito, mawasiliano n.k yanavutia wanunuvi na kuhakikisha bei nzuri masokoni | 160 |

| | | | | |
|-----------------------|----------|---------------|--|-----|
| Value addition | 16/07/18 | all districts | Ongeza thamani na kuhakikisha ubora na bei nzuri sokoni, usianike maharage ardhini, yatandaze kwenye turubai. Chambua kupata punje bora zenyе rangi zinazofanana | 160 |
| Nutrition | 17/07/18 | all districts | Tumia kwa chakula maharage ya JESCA (kijivu/kombati/Punda) Selian 14 na 15 yana madini ya chuma na zinki ambayo ni muhimu kwa watoto, wajawazito na wazee | 158 |
| Value addition | 18/07/18 | all districts | Ongezea thamani, kipato na panua wigo wa ulaji kwa kutengeneza bidhaa za maharage kama unga wa lishe, biskuti, maandazi nk. Wasiliana na afisa lishe wa wilaya | 157 |